

## URASIMISHAJI RASILIMALI ARDHI MIJINI

Mpango wa Kurasismisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) ni sehemu ya jitihada za Serikali ya Tanzania katika kupunguza tatizo la kuwepo kwa rasilimali ardhi na majengo mijini zinazomilikiwa katika mfumo au sekta isiyo rasmi. Hali hii inawafanya wamiliki wa rasilimali ardhi mijini kukosa fursa mbalimbali za kukuza na kuendeleza mitaji kwa kutumia mali hizo. Hii inajumuisha ardhi na mali za majengo yaliyo katika maeneo yasiyopimwa na ambayo hayana hati miliki inayotambuliwa kisheria.

Urasimishaji rasilimali ardhi mijini ni pamoja na kuwezesha umiliki wa ardhi uliopo kwa baadhi ya wamiliki wa maeneo yasiyo rasmi uwe na uhai na nguvu inayotambulika kisheria kwa:

- Kupanga na kupima ardhi na kuipa uhai wa kisheria rasilimali ardhi kulingana na kanuni na sheria zilizopo,
- Kuhakiki na kupima rasilimali ardhi kwa kuziwekea alama maalum kwa mujibu wa kanuni na taratibu zilizowekwa kisheria
- Kusajili umiliki wa rasilimali ardhi katika nyaraka/ rejesta zilizowekwa kisheria ili kuwezesha umiliki kutoka katika mfumo usio rasmi na kuwa na umiliki ulio rasmi uliowekwa kwa mujibu wa sheria za kiutawala

### *Manufaa na Umuhimu wa Kurasimisha Ardhi Mijini:*

Urasimishaji wa rasilimali ardhi mijini unawawezesha wamiliki kunufaika kijamii na kiuchumi kutokana na utaratibu huu wa;

- Kushirikisha wananchi katika kupanga na kupima ardhi pamoja na kuboresha maeneo ya makazi wanayomiliki.
- Kupunguza migogoro ya ardhi isiyo ya lazima ikiwemo ile ya mipaka na uvamizi wa viwanja,
- Kuwa na uhakika wa usalama wa miliki inayotambulika kisheria
- Kuwa na miliki inayotambulika kisheria katika uwanda na mtandao mpana zaidi ya ndugu, jamaa na majirani na thamani yake kuongezeka zaidi
- Kuwa na rasilimali ardhi inayoweza kutumika kama nyezo ya kujipatia fursa zaidi kiuchumi ikiwa kama dhamana katika kupata mikopo, uwekezaji, kununua na kuuza hisa ili kuongeza mtaji
- Kuongezeka kwa thamani ya ardhi kutokana na kutambulika kisheria,
- Kusaidia kudhibiti ongezeko la ukuaji wa ujenzi wa makazi holela na uharibifu wa mazingira, pamoja na kupunguza msongamano wa watu na makazi pamoja na uwezekano wa majanga ya moto au magonjwa ya milipuko

***Urasimishaji rasilimali ardhi mijini ni pamoja na kuwezesha umiliki wa ardhi uliopo kwa baadhi ya wamiliki wa maeneo yasiyo rasmi uwe na uhai na nguvu inayotambulika kisheria***

- Kupata taarifa sahihi juu ya umiliki wa ardhi mijini
- Kuchangia upatikanaji wa mapato katika ngazi ya kaya na taifa na hatimaye kupunguza umasikini wa kipato.

Lengo la MKURABITA katika urasimishaji rasilimali mijini ni pamoja na:

- Kuanzisha na kuwezesha utekelezaji wa mfumo shirikishi wa urasimishaji rasilimali mijini ambao wadau wake muhimu ni wamiliki wa rasilimali ardhi pamoja na majengo yanayomilikiwa katika sekta isiyo rasmi, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi za fedha na wawezeshaji wa utaalum na teknolojia zikiwemo wizara za kisekta
- Kuibua mchakato endelevu wa urasimishaji wa rasilimali ardhi mijini unaotekelezwa kwa awamu ukifungamana na ujengaji uwezo wa wamiliki na uwezeshaji wa kiuchumi kwa kuwaunganisha na huduma za upatikanaji na ukuzaji wa mitaji.
- Kuwezesha uwepo wa kasi ya urasimishaji kwa kupunguza urasimu unaosababisha gharama kubwa kwa walengwa na usimamizi wa utekelezaji wa urasimishaji wa biashara kwa kukasimu baadhi ya madaraka ya wizara na mamlaka za urasimishaji kwa watendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa husussan Halmashauri za Miji, Manispaa na Majiji.

### *Shughuli za MKURABITA Katika Urasimishaji wa Rasilimali Ardhi Mijini:*

MKURABITA imebuni mbinu shirikishi iliyojikita katika kujenga uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, walengwa na wadau wengine nchini ili kufanikisha urasimishaji rasilimali ardhi mijini. Hivyo MKURABITA inaendelea:-

- Kuhamasisha wananchi na viongozi ngazi ya mkoa, wilaya, kata, mtaa ili kuwa na uendelevu na usimamizi wa urasimishaji katika maeneo yao,
- Kuhamasisha wananchi hususan wamiliki wa rasilimali ardhi mijini zilizo katika mfumo usio rasmi kushiriki na kuchangia gharama za urasimishaji,
- Kuhamasisha wananchi kushirikiana na wataalam katika upangaji wa maeneo ya utekelezaji wa kazi za urasimishaji na uboreshaji wa makazi,
- Kujenga uwezo wa Halmashauri za Miji, Manispaa na Majiji kwa kutoa mafunzo na vifaa maalum kwa zoezi la urasimishaji ili kusimamia utekelezaji wa urasimishaji endelevu katika halmashauri husika.

Aidha katika utekelezaji wa mchakato huu MKURABITA kwa kushirikiana na wananchi pamoja na mamlaka za halmashauri husika zinazingatia hatua zifuatazo:

- Uhamasishaji wa walengwa, viongozi wa Serikali za Mitaa na wadau wengine,
- Utoaji mafunzo maalum kwa timu ya wataalam kutoka Halmashauri za Miji, Manispaa na Majiji,
- Utambuzi miliki, upimaji na utayarishaji wa hifadhi data (Database),
- Uandaaji wa michoro ya mipango miji, ambapo wamiliki kwa kushirikiana na wataalam hupisha/huachia sehemu ya maeneo yao kwa matumizi ya kijamii, na hatimaye upimaji ardhi kufanyika kulingana na mpango ulioandaliwa kwa pamoja na wadau,
- Utayarishaji wa ramani za upimaji
- Uidhinishaji wa michoro ya mipango miji na ramani za upimaji. Michoro ya Mipango Miji huidhinishwa na Mkurugenzi wa Mipango Miji na Vijiji kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ramani za Upimaji huidhinishwa na Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi baada ya Michoro ya Mipango Miji kuidhinishwa,
- Utayarishaji wa Hati Miliki za rasilimali ardhi hufanywa na wataalam katika halmashauri baada ya wamiliki kuwasilisha maombi ya umiliki, Afisa Ardhi Mteule wa halmashauri huidhinisha na kupeleka kwa Kamishna Msaidizi wa Kanda kwa usajili,
- Utaoaji wa Hati Miliki kwa wamiliki wa rasilimali ardhi hufanyika baada ya usajili kukamilika kwa Kamishna Msaidizi wa Kanda, kabla ya kukabidhiwa Hati Miliki, wamiliki hulipia gharama zote za urasimishaji kama ilivyokubalika katika vikao vya uhamasishaji,
- Kuwajengea uwezo wamiliki wa rasilimali ardhi mijini kupitia mafunzo, juu ya upatikanaji na urejeshaji wa mikopo kwenye mabenki na vyombo vingine vya fedha,
- Kwa kushirikiana na wadau, MKURABITA huhamasisha wananchi juu ya uboreshaji wa maeneo yaliyorasimishwa ikiwa ni njia ya usimamizi endelevu wa mipango iliyowekwa.

### *Maeneo yaliyofikiwa na MKURABITA:*

Kupitia utaratibu na mbinu mbalimbali zilizobuniwa na MKURABITA katika kujenga uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, baadhi ya halmashauri za miji na manispaa zimenufaika na Mpango huu. Halmashauri hizo ni pamoja na Halmashauri ya Mji wa Njombe, Mji Mdogo wa Tunduma, Manispaa ya Morogoro na Arusha. Lengo la MKURABITA ni kuhakikisha zoezi la urasimishaji ardhi mijini linakuwa shirikishi na linatekelezwa kwa kasi na gharama nafuu.

MKURABITA

**Kwa maelezo zaidi Wasiliana na Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya Au:**
**• Kitalu Na. 20 • Ocean Road • S.L.P. 7975 • DSM • Tanzania • Simu: +255 22 2126250/3**
**Nukushi +255 22 2126252 • Barua Pepe: info@mkurabita.go.tz • Tovuti: www.mkurabita.go.tz •**